# KUWAZIA YALIYO MEMA KULINGANA NA NENO

*Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na kristo, yatafuteni yaliyo juu, kristo aliko ameketi mkono wa kuuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu siyo yaliyo katika nchi.kwa maana mlikufa na uhai wenu umefichwa pamoja na kristo katika Mungu (wakolosai 3:1-3)*

Mkumbuke Yesu Kristo niani mwako (2 Tim 2:8) " mambo yoyote yaliyo yakweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza , yoyote yenye sifa njema, ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote yatafakarini hayo (wafilipi 4:8). Sasa, ni jambo la ajabu sana kwamba hili hufikiriwa na watu wengi wanasema " vema, mimi ni mdhaifu, imani yangu siyo nyingi, mimi siyo mkristo mzuri sana " hivyo ndivyo shetani anavyopenda useme. Hapo sasa unazungumza lugha yake unaona? Hupaswi kamwe kusema hivyo. Usiache ushuhuda wako uwe kinyume (hasi) uache uwe mwema (chanya) wakati wote "Nimeokolewa ninaye Mungu moyoni mwangu. Namwamini yeye kwa moyo wangu wote, " Je unaamini uponyaji wa Kiungu? Naamini kwa moyo wangu wote.

Uache ushuhuda wako siku zote na mawazo yako, kila kitu……… kamwe usiruhusu mawazo yaliyo kinyume yaje niani mwako kama unaweza kujifanya hivyo inapo anza hilo, usiruhusu likae hapo, vema unasema siwezi kuyazuia mawazo yasije. " Kizuri hiyo ni kama Yule mkulima ambaye alisema siwezi kuwazuia ndege kuja shambani mwake, lakini kwa hakika anaweza kuwazuia wakiwa wanakaa hapo kujenga viota. "Sasa hilo ni jambo zuri, unaona hilo ni jambo zuri. Unaona hilo? Huwezi kuyazuia mawazo yanapokuja lakini usiyakaribishe yatue. Vitu vyote ni vyangu kupitia Mungu (1 kor 3:23) na mtenda huyahifadhi hayo.

Na Mungu anaweza tuu, kukubariki wewe unapokiri kuwa amekufanyia wewe hayo, unaona. Yeye ni kuhani mkuu wa maungamo yetu, ni sawa hiyo? (waebrania3: 1-2) Yeye amesema kuwa ni kuhani mkuu wa maungamo yetu (waebrania 4:14-16) anaweza hutufanyia hayo tuu kwa kadiri tunavyoyakubali hayo, na kuyaamini na kuyaungama hayo [1]

Nimewaona watu wanakuja mimbarini nami ningesema "Unaamini wewe? Oh ninayo imani yote ndugu Branhom. Sasa, simaanishi kuwafanya wao duni. Naliheshimu hilo lakini wanapaswa kuwa juu hapa, na wako mbali hapa chini lakini unajua ni nini hiyo? Nitumaini badala ya imani. Imani inafanyakazi hapo hapo. Sasa tumaini linatumainia hilo, lakini imani imeshafanya hilo(waebrania 11:1-3). Imani halisi inalifanya hilo unaona, tuna matumaini mengi lakini hatuna imani ya kutosha. Kwa hiyo tunataka kubadilika leo kutoka tumaini kwenda kwenye imani halisi. Na kuna njia moja tu iwezayo kutupa imani halisi, hiyo ni kwa kufikiri mambo mema kwa vitu vyema [2]

Na leo, tunapomwamini Mungu kwa moyo wetu wote na kumkabidhi mwana wake, Bwana Yesu, na Mungu anatambua hiyo imani kwamba ni ya kweli kwake, hapo anatuma huku chini Roho Mtakatifu wa ahadi na kututia muhuri sisi mpaka siku yetu ya ukombozi , jamani hakuna mawazo (hasi) kinyume hata kidogo katika ukristo kila kitu ni kazi iliyokwisha fanywa tayari imemalizika.

Uponyaji siyo kile kitu anaweza kufanya. Ni Kile Mungu alichofanya unaona? Ni kazi iliyokwisha (Yohana 19:30) Wokovu siyo kile ntu awezacho kufanya, kile kanisa linachoweza kufanya, ni kazi iliyomalizika na imani yako katika kazi ile iliyomalizika ambayo Kristo alimaliza kila kitu kilichoingizwa katika anguko, kristo alimaliza kila kitu kilichoingizwa katika anguko, Kristo alikikomboa hicho na kukirudisha kupitia upatanisho wa mauti yake, mateso yale makuu pale msalabani. Naye aliwekwa kaburini, na Mungu akamfufua yeye siku ya tatu kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu.

Na sasa tunamuona yeye ameketi mkono wa kuume wa Mungu akifanya upatanisho kwa kukiri kwetu au Neno hilo hilo linatafsiriwa" maungamo yetu" na haijalishi umeomba sana kiasi gani, ulie sana kwa kiasi kikuu, uomboleze kwa kiasi gani, kwa kiasi gani ufanye vyovyote haitakubaliwa kamwe. Mungu hawezi kukufanyia chochote mpaka kwanza umekikubali kwa imani, na kiliamini hilo na ukaliungama hilo, hiyo ndiyo njia pekee Mungu awezayo kufanya sasa ni mpaka wewe utende kwanza kwa sababu Yeye ni kuhani mkuu

fanya upatanisho juu ya maungamo ya imani ya roho katika kazi ile iliyomalizika. Siamini kama kuna yoyote awezaye kupata kosa na jambo hilo. Unaona? Huo ndio msingi wa uponyaji wa kiungu. [3]

Unapo anza kufikiri juu ya uponyaji wa kiungu uende ufikiri juu ya Kristo …………muweke yeye katika nia yako "kama kuna sifa zozote kama kuna wema wowote" Biblia inasema, (wazia) fikiria mambo hayo (wafilipi 4:8).

Kama wazo lolote linakuja, vema pengine haiwezi kuwa hivyo, pengine…………liondoe mawazoni mwako haraka sana. Fikiria mambo yaliyo mema, usiache mawazo (hasi) kinyume yapite hapo usiyaache yasimame kwa vyovyote. Kama yanaanza wazia mema (chanya) Yesu.

Usifikirie, kukaa pale kwenye kiti cha ulemavu wewe, kwamba hakuna matumaini. Huwezi kusaidiwa sivyo hivyo usiruhusu mawazo mabaya (hasi) kinyume yapite hapo. Usiyaache yaweke nanga. Huwezi kuzuia yasipite akilini mwako (hiyo ni kweli) lakini usiyaache yatue/kusimama hapo [4]

Nafikiri hilo ndilo tatizo kuu la watu wa leo tuna mambo mengi sana katika akili (nia) zetu (2 kor 11:1-3). Hata tunapofika kwenye huduma ya uponyaji tunaonekana kufikiri "vema sikupata kadi ya maombi usiku wa leo" au pengine "sitaweza kuombewa" hatutaweza kufanikisha mengi ili mradi tunafikiria mawazo ya aina hiyo"

Hebu tuwaze mema (chanya) katika mawazo yetu [5]

Na unajua mara nyingi tunapomfikiria Mungu niani mwetu na kuweka akili zetu kwa Mungu hapo Mungu huja karibu na sisi [5]

Unasikia mambo mengi sana leo juu ya kuwaza mema (chanya) unaweka tuu akili yako kwenye kitu chochote na unafikiri mema (chanya) juu ya hicho, shetani anaweza kufanya hivyo, kuna kitu kimoja tuu kinachotawala juu ya vyote na hicho ni Neno la Mungu kama unafikiri kinyume na Neno, sahau fikira za mawazo yako fikiria juu ya Neno [6]

Vema hivyo ndivyo afanyavyo shetani. Anatuburuza chini kwa kila kitu na analionyesha kuwa linapendeza, na anaingia ndani na kukubaliana na kila kitu pamoja na karibu kila Neno la Mungu, lakini hawezi kuchukuwa Neno lote la Mungu. Hivyo ndivyo tupaswavyo kufanya, atasema naamini kuwa kuna kitu kama kuzaliwa mara ya pili, lakini ninavyofikiria ni badiliko la akili (nia).

Lakini siyo badiliko la akili (nia,) kuwa kiumbe kipya. Kanisa halihitaji kuinua sura linahitaji badiliko. Inahitaika iwe ni kiumbe kipya (2 kor 5:17) [7]

Sasa huyu Roho Mtakatifu anapowakilisha kama tai arukaye juu ya nchi na kumpa huyo mwaminio…… "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu. Hakuna mtu awezaye kuja kwangu kwa kupenda kwake mwenyewe " Siyo mawazo yako ufikiriyo siyo kuweza kwako ni Mungu aliye huvuta Yohana (Mt 6:39,44) unaona, unaona? " Wote alionipa Baba watakuja kwangu"

Sasa Roho Mtakatifu yuko hapa duniani aliangalia wale watu binafsi ambao Mungu amewakusudia uzima katika wakati huu (Matendo 13: 48) na mara anapowapata inafanya kama ilivyofanya ndani ya Yesu Kristo, Yule mwana mkuu wa Mungu. Yeye aliyetukomboa sisi sote inakuja na kuchukuwa mahali pale pakukaa ndani ya maisha ya mwanaadamu [8]

Katika mambo yote omba. Mtu fulani alikuja hapa siku moja na akasema ndugu Branham, unafikiri nisahihi kufanya jambo fulani?

Nikasema kwanini unajiuliza swali juu ya hilo? Unaona? Kama kuna swali katika akili yako, liache pekee usilifanye hata kidogo, kaanalo hilo unapoanza kufanya chochote na kama kuna maswali hata kama ni sahihi au siyo sahihi kaa mbali nacho usikifanye kabisa hapo sasa utajua uko sahihi.

Sasa mambo yote tuyachukue kwanza kwa maombi utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake yote na mambo yote mtazidishiwa. (Matayo 6:33). Ninaamini kabisa pasipo shaka kama wanaume na wanawake wataweza kufikia kiwango kwenye nafsi zao mawazo yao na mtazamo wao utakuwa mkamilifu mbele za Mungu, hilo litakuwa kanisa lenye nguvu sana lililo wahi kuwapo [9]

Nikaribieni ninyi nami nitawakaribia ninyi asema Bwana (Yakobo 4:8) kama tungeweka akili zetu mbali na mambo ya dunia na upumbavu mwingi ambao hatuna budi kufikiria huo. Na mawazo ya moyo wangu yapate kibali mbele zako Ee Bwana (zab 19:14)

Ikiwa katika ile ista (Pasaka) ya kwanza wakati wale mitume wawili, cleopa na rafiki yake, walikuwa njiani akawasogelea alitokea porini na akaanza kuzungumza nao…….. na halafu akajitambulisha kwao kwa kutenda muujiza kama alivyofanya tuu kabla ya kusulubishwa nao wakakimbia haraka na kurudi nyuma na kusema hakika, Bwana amefufuka na ametutokea sisi (Luka 24:13-35)

Sasa Maria alikuwa akimfikiria yeye na alivyokuwa akiendelea kwa ghafla aliinua kichwa chake tena. Alikuwa na uhakika wakati huu kwani karibu naye, ilisimama nuru kuu, pengine ni nguzo ile ile ya moto iliyo waongoza Musa kule jangwani na (watoto) wana israeli. Akitembea kutoka ndani ya ile nuru, pengine iling'ara kuliko jua. Akatokea Yule malaika mkuu Gabriel naye akasema, " Salaam, Maria (Kwa maneno mengine "simama") umebarikiwa wewe miongoni mwa wanawake wote, kwa maana umepata neema kwa Mungu (Luka 1:26-38) [10]

Kama unataka Malaika wa kutokee wewe weka mawazo yako kwa Mungu na mbali na mambo ya dunia (Waebrania 1: 14). Nenda katika kazi zako, nenda kanisani, nenda katika uoshaji wa vyombo vyako popote ulipo, weka mawazo yako kwake, mchana wote na usiku wote (zab 16:8). Hapo sasa Mungu atafanya kitu fulani, unasogea karibu naye dunia imefungiwa nje, wewe tu na yeye mpo pamoja [11]

Sasa, fikiria tunamaanisha hilo, kila kitu kimesalimishwa " Siyo mimi niwazaye mwenyewe. Siendi kufikiri kama ninavyofikiri, Bwana ninaenda kuwaza kama wewe. Na ume ahidi kuwa nimeponywa nafikiri hilo nasalimisha mawazo yangu, sitafikiria tena juu ya ugonjwa wangu sitafikiria juu ya magonjwa niliyokuwa nayo, sitafikiria juu ya chochote ila nifikiri juu ya ulichosema

Ndugu Braham anaendelea sasa, hapo mbele yako amesimama mtu kama ulivyokuwa dakika chache zilizopita, ulikuwa mgonjwa chini pale, lakini kuna mtu mzima kupitia huyu, sasa wewe tuu kwa imani ufunge macho yako, endelea mbele kwa ule mwili ulio mzima na endelea kutembelea na uendelee mbele (2 kor 3:18) [12]

Nukuu za kiingereza

[1] Sheria (55 - 0115) aya E 18
[2] Nafasi ya mwaminio ndani ya Kristo (55 – 0227 A), Aya E-25
[3] Jehova jire (56 – 1209 E), Aya E 18-19
[4]Kipofu Bartimayo(55-1115) aya E-29-30
[5] Imani ya maria (59 - 0409), Aya E-9
[6] Kwa nini ilikuwa ni wachungaji (64 - 1221) aya 70
[7] Kutokuamini hakumzuii Mungu (62 - 0128) aya E – 35
[8] Muhuri ya pasaka (65 - 0410), Aya 85-86
[9] Roho zinazoshawishi (55)- 0724 , Aya 43-45
[10] Neno la Mungu lisilobadilika (60 - 0724), aya, E – 37-38
[11] Mungu wa miujiza (59 -1126), Aya – 24
[12] Nenda ukamwamshe Yesu (63- 1130 E), Aya 274

Jiwe la kujengea la kiroho nambari 107 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa saa hii, yamekusanywa na Gerd rodewald friendestr. 69.D-75328 Schomberge Germany Simu (+49) 2357613 Fax 72353306.

---

Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Bibilia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho uk.)

---

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa: Charles E. Y. Kanju

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0713230098*